



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

A large circular graphic containing a map of Tanzania. The map is filled with a scenic image of Mount Kilimanjaro with snow-capped peaks, a giraffe, and a lion. The text '2022 Takwimu za Msingi Tanzania' is overlaid on the map in large, bold, white letters with a blue outline.

# 2022 Takwimu za Msingi Tanzania



Ofisi ya Taifa ya Takwimu  
Wizara ya Fedha na Mipango  
Dodoma






**Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

“Bila kuwa na takwimu huwezi kushughulikia changamoto za ajira, matatizo ya watu wenye mahitaji maalum, kutoa huduma za kijamii wala kuleta maendeleo”, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hafla ya uzinduzi wa Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 jijini Dodoma, Septemba 2021”.





Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi wakati wa uzinduzi wa Mkakati wa Uelimishaji na Uhamasishaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, jijini Dodoma



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)-(kulia.) na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman Abdulla (MBW)-(kushoto) wakizindua Ripoti ya Mgawanyo wa idadi ya Watu kwa Maeneo ya Kiutawala na Ripoti ya Mgawanyo wa Idadi ya Watu kwa Umri na Jinsi kutokana na Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Zanzibar

# YALIYOMO

Dibaji .....	ii
<b>BAADHI YA MAFANIKIO MUHIMU YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA .....</b>	<b>iii</b>
<b>TAARIFA MPYA KWA MWAKA 2022 .....</b>	<b>xxi</b>
Vifupisho, Visawe, Alama na Tanbihi .....	xxxiii
1.0 Usuli .....	1
2.0 Jiografia .....	2
3.0 Siasa .....	14
4.0 Idadi ya Watu .....	20
5.0 Afya .....	25
6.0 Elimu .....	31
7.0 Ajira .....	35
8.0 Uwekezaji .....	37
9.0 Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi (HBS) .....	39
10.0 Viashiria vya Uchumi .....	42
11.0 Biashara ya Nje .....	51
12.0 Viashiria vya Utendaji kwa Baadhi ya Shughuli za Kiuchumi .....	53
12.1 Mifugo .....	53
12.2 Madini .....	54
12.3 Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani .....	55
12.4 Umeme .....	56
12.5 Usafirishaji .....	57
12.6 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano .....	63
12.7 Fedha za Serikali .....	66
13.0 Takwimu za Uhalifu Tanzania .....	67
14.0 Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) Tanzania .....	70
15.0 Kuagiza, Maelezo na Maktaba .....	77

## Dibaji

Kijitabu cha Takwimu za Msingi cha Tanzania mwaka 2022 kinatoa picha ya hali halisi ya mwenendo katika nyanja za uchumi, jamii, mazingira na siasa. Kitabu hiki kinawasilisha mtiririko wa takwimu kuanzia mwaka 2018 hadi 2022.

Kijitabu hiki kina takwimu kutoka vyanzo mbalimbali vya taarifa kutoka machapisho ya takwimu rasmi yanatolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Wizara, Idara na Wakala nyingine za Serikali. Taarifa za takwimu zilizowasilishwa ni muhimu kwa kupanga mipango, kufuatilia na kutathimini programu mbalimbali za maendeleo katika ngazi zote za kiutawala.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu kama mratibu na mzalishaji wa takwimu rasmi nchini inathamini michango inayotolewa na wadau mbalimbali wa takwimu katika utoaji wa takwimu zinazotumika katika uandaaji wa kijitabu hiki. Ili kushiriki kikamilifu katika kuimarisha Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu tunaomba ushirikiano udumishwe katika kuhisha taarifa na kuandaa makala zijazo za vijitabu kama hiki na machapisho mengine ya kitakwimu.

Takwimu za karibuni za mwaka 2022 zilizowasilishwa katika kijitabu hiki kwa baadhi ya viashiria ni za awali, na baadhi viashiria vimefanyiwa mapitio kulingana na sera za mapitio za Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Aidha, taarifa za baadhi ya majedwali zinatokana na Sensa na tafiti ambazo kwa kawaida hufanyika katika vipindi vya miaka kumi au mitano. Kijitabu hiki kinajumuisha takwimu halisi za viashiria vya watu na makazi kutokana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022. Mapengo ya takwimu yaliyomo katika kijitabu hiki na yanayonasibishwa na sensa na tafiti yatapatikana kwenye taarifa husika zitakapopatikana.










Tunakaribisha maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau yatakayoboresha makala ijayo ya Takwimu za Misingi Tanzania.

Nakala laini ya kijitabu hili inapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu; [www.nbs.go.tz](http://www.nbs.go.tz). Kwa mahitaji ya taarifa za ziada na takwimu zilizochapishwa tafadhali tembelea Maktaba na tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu.





# BAADHI YA MAFANIKIO MUHIMU YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA



-  Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022
-  Sensa ya Majengo
-  Anwani za Makazi
-  Sekta ya Afya
-  Sekta ya Elimu
-  Sekta ya Maji
-  Sekta ya Kilimo
-  Sekta ya Utalii
-  Sekta ya Ujenzi


# 1. Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022





*Je, ni yapi matokeo makuu ya Sena ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022?*


*Tuko watu milioni 61.7, wanaume milioni 30.1 na wanawake milioni 31.6*



Je, ni nini manufaa muhimu ya Sensa?

Yanasaidia kujua tuko wangapi, kupanga mipango yenye kuzing atia Ushahidi wa kitakwimu, kutoa huduma stahiki kwa jamii kama vile hospitali, shule, miundo mbinu, pamoja na kuwezesha taasisi binafsi kupanga, kufuatilia na kutathmini programu zao za uwekezaji

## 2. Sensa ya Majengo



Je, unafahamu nini kuhusu Sensa ya Majengo ya mwaka 2022?

Ni Sensa ya kwanza ya Majengo kufanyika nchini. Sensa hiyo itaisaidia Serikali kutambua idadi na aina ya majengo yaliyopo ili kuweka mikakati ya kupata nyumba na makazi bora

### 3. Anwani za Makazi



Vilevile, kwa mara ya kwanza Serikali iliweza kuanzisha Anwani za Makazi nchini zitakazowezesha utambuzi wa majengo na ufikishaji huduma kwa wananchi.

## 4. Sekta ya Afya



- ✚ Serikali ilipokea mkopo nafuu wa Shilingi trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa ajili ya kukabiliana na athari za UVIKO-19. Fedha hizo zimetumika kujenga miundo mbinu ikiwemo vituo vya afya, ununuzi wa vifaa tiba, na dawa.
- ✚ Kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi na ukarabati wa hospitali za rufaa, kikanda na mikoa; kuendelea na ujenzi wa hospitali 59 za halmashauri na ukarabati wa hospitali kongwe 19 za halmashauri; na kuendelea na ukamilishaji wa zahanati 300.

## 5. Sekta ya Elimu



- ✚ *Kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi katika vyyo vya elimu ya juu kutoka 87,934 (2020/21), 106,620 (2021/22) na 113,383 (2022/23)*
- ✚ *Ongezeko la fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kutoka Shilingi bilioni 464 (2021/22) hadi Shilingi bilioni 654 (2022/23)*
- ✚ *Ujenzi wa Vyyo vipya vya Elimu na Mafunzo ya ufundi stadi*
- ✚ *Ujenzi wa shule mpya za sekondari na msingi*
- ✚ *Ujenzi wa madarasa ya ziada 15,000 kutokana na fedha za UVIKO-19*



## 6. Sekta ya Maji



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizindua Mradi wa Maji wa Kakonko – Kiziguzigu mkoani Kigoma**

- ✚ *Miradi 1,197 ya usambazaji maji imekamilika ambapo vijiji vipya 2,056 vimeanza kupata huduma bora ya maji, na zaidi ya Shilingi bilioni 400 zimetumika katika miradi hiyo.*
- ✚ *Upatikanaji bora wa maji vijijini [70.1% (2021) – 74.5% (Februari 2023)].*
- ✚ *Upatikanaji bora wa maji mijini [84% (2021) – 86.5% (Februari 2023)].*

## 7. Sekta ya Kilimo

🇰🇪 Ongezeko la bajeti ya Serikali kwa ajili ya kilimo (kutoka Shilingi bilioni 254 hadi karibu Shilingi trillion 1)



🇰🇪 Mbolea ya ruzuku tani 268,000 zilinunuliwa na wakulima, yenye thamani ya Shilingi bilioni 634.5

## 8. Sekta ya Utalii



*Mapato yatokanayo na utalii yaliongezeka kutoka dola za kimarekani 1,310 mwaka 2021 hadi dola za kimarekani milioni 2,527 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 93. Je, unadhani ongezeko hilo lilitokana na nini?*

*Haya ni matokeo ya juhudi za kipekee za Mh. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhamasisha utalii kupitia filamu maalumu ya Royal Tour, ambayo kwa kiwango kikubwa iliongeza idadi ya watalii waliokuja nchini kutoka watalii 922,692 mwaka 2021 hadi 1,454,920 (58%) mwaka 2022*

## 9. Sekta ya Ujenzi

Ujenzi wa daraja la Kigongo-Busisi, Mwanza (km 3.2) umefikia asilimia 70



Daraja la Tanzanite, Dar es Salaam (km 1.03) limekamilika



🇲🇵 Daraja la Wami, Pwani lenye urefu wa mita 513.5 limekamilika



🇲🇵 Ujenzi wa kilomita 112.3 za mradi wa barabara ya mzunguko wa nje jijini Dodoma unaendelea



✚ Ujenzi wa barabara ya Tabora–Koga–Mpanda  
(km 342.9) umekamilika



✚ Ujenzi wa barabara ya Kibondo–  
Kasulu–Manyoni (km 260.6)  
unaendelea



✚ Ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere (JNHPR) wa megawatt 2,115 unaendelea na umefikia zaidi ya asilimia 80



✚ Ujenzi wa awamu ya pili wa Mji wa Serikali wa Magufuli jijini Dodoma umefikia asilimia 60



- Ujenzi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika ya Mashariki (EACOP) kutoka Hoima (Uganda) hadi Chongoleani, Tanga (Tanzania) unaendelea.



- Kuendelea na mchakato wa ujenzi wa mtambo wa kuchakata na kusindika gesi asilia, Lindi.



Muonekano wa kisanifu wa eneo la mtambo



## Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR)



- ✚ Kipande cha Dar es Salaam–Morogoro (Ujenzi umefikia asilimia 97.91)
- ✚ Kipande cha Morogoro–Makutupora (Ujenzi umefikia asilimia 92.23)
- ✚ Kipande cha Makutupora–abora (Ujenzi umefikia asilimia 4.59)
- ✚ Kipande cha Tabora–Isaka (Ujenzi umefikia asilimia 0.66)
- ✚ Kipande cha Isaka–Mwanza (Ujenzi umefikia asilimia 25.75)
- ✚ Kipande cha Tabora-Kigoma (Mkandarasi amepatikana)

*Ujenzi wa Meli ya MV Mwanza unaendelea na umefikia zaidi ya asilimia 80*



# TAARIFA MPYA KWA MWAKA 2022

## Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022

Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imetimiza wajibu wake wa kufanya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kama ilivyofanyika katika awamu nyingine zilizopita. Sensa zilizopita zilifanyika miaka ya 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012. Sensa ya mwaka 2022 imefanyika kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu SURA 351 ambayo inaelekeza Serikali kufanya Sensa ya Watu na Makazi kila baada ya miaka kumi. Aidha, Sensa imefanyika kukidhi matakwa ya kimataifa ambapo Umoja wa Mataifa unazitaka nchi kufanya Sensa ya Watu na Makazi angalau mara moja ndani ya miaka kumi.

Sensa ya mwaka 2022 limeratibiwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) Zanzibar kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Zanzibar; Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu-UNFPA, Ofisi ya Sensa ya Marekani na Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhamaji-IOM.

Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 yatasaidia kupanga mipango jumuishi, maendeleo endelevu ya nchi na yataongeza uwazi katika kugawa rasilimali zilizopo kuendana na uwiano wa idadi ya watu katika ngazi zote za utawala. Halikadhalika, matokeo yatatumiwa na Serikali na wadau wengine katika kufuatilia na kutathmini mipango mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kama vile Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050; Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (mwaka 2021/22-2025/26) na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (2021/22 -

2025/26), Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050, Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030.

Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 yameonesha kuwa kati ya watu 61,741,120 waliohesabiwa mwaka 2022 katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanaume ni 30,053,130 sawa na asilimia 49 ya watu wote nchini na wanawake ni 31,687,990 sawa na asilimia 51.

#### **Mgawanyo wa Idadi ya Watu kwa Eneo na Jinsi, Tanzania, 2022**


<b>Eneo</b>	<b>Idadi ya Watu</b>	<b>Wanaume</b>	<b>Wanawake</b>
<b>Tanzania</b>	<b>61,741,120</b>	<b>30,053,130 (48.7%)</b>	<b>31,687,990 (51.3%)</b>
Tanzania Bara	59,851,347	29,137,638 (48.7%)	30,713,709 (51.3%)
Tanzania Zanzibar	1,889,773	915,492 (48.4%)	974,281 (51.6%)

Chanzo: Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Tanzania

Wastani wa kasi ya ongezeko la idadi ya watu kwa mwaka nchini Tanzania imeongezeka kutoka asilimia 2.7 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 3.2 mwaka 2022.

Idadi kubwa ya watu Tanzania wana umri mdogo, ambapo asilimia 42.8 wana umri chini ya miaka 15. Asilimia ya idadi ya watoto wenye umri chini ya miaka 15 imepungua kidogo kutoka asilimia 43.9 katika Sensa ya Mwaka 2012 hadi asilimia 42.8 katika Sensa ya Mwaka 2022.


## Mgawanyo wa Asilimia ya Watoto (miaka 0-14); 2002, 2012 na 2022



Chanzo: Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022

Watu walio chini ya umri wa miaka 18 kwa Tanzania ni asilimia 49.0 ambayo ni karibu sawa na Tanzania Bara lakini ni pungufu kidogo kwa Tanzania Zanzibar ambayo ni asilimia 47.2.


## Mgawanyo wa Asilimia ya Watu (miaka 0-17); Tanzania 2022



Chanzo: Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022

Asilimia ya vijana wenye umri wa miaka 15-35 imepungua kidogo kutoka asilimia 34.7 katika Sensa ya Mwaka 2012 hadi asilimia 34.5 katika Sensa ya Mwaka 2022. Hali kama hii imeonekana pia kwa Tanzania Bara. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, asilimia ya vijana imeongezeka kidogo kutoka asilimia 36.20 kwa Sensa ya Mwaka 2012 hadi asilimia 37.03 kwa Sensa ya Mwaka 2022.

### Mgawanyo wa Asilimia ya Vijana (miaka 15-35); 2002, 2012 na 2022



Chanzo: Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022

Asilimia ya watu wenye umri wa kufanya kazi (miaka 15-64) nchini imeongezeka kutoka asilimia 52.2 mwaka 2012 hadi asilimia 53.4 mwaka 2022. Mwenendo huu unafanana kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

### Mgawanyo wa Asilimia ya Watu wenye Umri wa Kufanya Kazi (miaka 15-64); Tanzania, 2012 na 2022

Eneo	2012	2022
Tanzania	52.2	53.4
Tanzania Bara	52.2	53.4
Tanzania Zanzibar	54.7	56.3

Chanzo: Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Tanzania

Asilimia ya wazee (miaka 60 na kuendelea) nchini imeongezeka kidogo kutoka asilimia 5.6 mwaka 2012 hadi asilimia 5.7 mwaka 2022 kwa Tanzania na Tanzania Bara. Kwa Tanzania Zanzibar, wazee wamebakia takriban asilimia tano ya watu wote.

**Mgawanyo wa Asilimia ya Watu wenye Umri wa Miaka 60 na Zaidi, Tanzania, 2012 na 2022**

Eneo	2012	2022
Tanzania	5.6	5.7
Tanzania Bara	5.6	5.7
Tanzania Zanzibar	4.5	4.5

*Chanzo: Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Tanzania*

**Sensa ya Majengo na Anwani za Makazi**

Matokeo yameonesha kuwa Tanzania ilikuwa na jumla ya majengo 14,348,372. Kati ya hayo majengo 13,907,951 (96.9%) yalikuwa Tanzania Bara na majengo 440,421 (3.1%) yalikuwa Tanzania Zanzibar.

**Idadi ya Majengo kwa Eneo, Tanzania, 2022**

Eneo	Idadi	Asilimia
Tanzania	14,348,372	100.0
Tanzania Bara	13,907,951	96.9
Tanzania Zanzibar	440,421	3.1

*Chanzo: Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Tanzania*

Vilevile, matokeo yameonesha kuwa majengo ya ghorofa ni 68,724, yasiyo ya ghorofa 13,540,363 na majengo yanayoendelea na ujenzi ni 739,285.

**Idadi ya Majengo Kwa Aina na Eneo, Tanzania, 2022**

Aina	Tanzania	Tanzania Bara	Tanzania Zanzibar
Majengo ya ghorofa	68,724	61,258	7,466
Majengo yasiyo ya ghorofa	13,540,363	13,152,298	388,065
Majengo yanayoendelea na ujenzi	739,285	694,395	44,890

*Chanzo: Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Tanzania*

Aidha, majengo 10,751,123 sawa na asilimia 74.9 yalikuwa na anwani za makazi na majengo 3,597,249 sawa na asilimia 25.1 hayakuwa na anwani za makazi kwa Tanzania nzima.

**Idadi ya Majengo kwa Hali ya Anwani za Makazi na Eneo, Tanzania, 2022**

Hali	Tanzania	Tanzania Bara	Tanzania Zanzibar
Majengo yenye Anwani za Makazi	10,751,123	10,406,722	344,401
Majengo yasiyo na Anwani za Makazi	3,597,249	3,501,229	96,020

*Chanzo: Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Tanzania*



## Matokeo Muhimu ya Utafiti wa Afya ya Mama na Mtoto na Viashiria ya Malaria (2022 TDHS-MIS)

Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022 (TDHS-MIS) ni utafiti wa Saba (7) kufanyika Tanzania kupitia programu ya DHS. Utafiti wa TDHS-MIS wa Mwaka 2022 ulifanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) Zanzibar na Wizara za Afya (MOH) kutoka Bara na Zanzibar kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (WAMJW), Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC), Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Lengo kuu la Utafiti wa TDHS-MIS wa Mwaka 2022 ilikuwa ni kupata taarifa za sasa za afya kwa ajili ya sera katika ngazi za kimataifa, kikanda na kitaifa na kupima hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, Mpango wa Taifa wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III 2021/22 - 2025/26), Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa mwaka 2021/22 hadi 2025/26, Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050 (EAC 2050), Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063 (ADA 2063) na Ajenda ya dunia ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2030). Vilevile matokeo ya utafiti huu pia yatasaidia kupima hatua iliyofikiwa katika kuboresha hali za maisha ya watu nchini.

Vifuatavyo ni baadhi ya Viashiria muhimu katika Utafiti wa TDHS-MIS wa Mwaka 2022:


### **Kiwango cha Uzazi (TFR)**

Kiwango cha uzazi ni wastani wa idadi ya watoto ambao mwanamke angeweza kuzaa kufikia umri wa ukomo wa kuzaa ikiwa angezaa watoto kulingana na viwango vya sasa vya uzazi.

- Ikiwa uwezo wa kuzaa usingebadilika katika viwango vya sasa, mwanamke nchini Tanzania angezaa wastani wa watoto 4.8 katika maisha yake.
- Kwa upande wa Tanzania Bara, uwezo wa kuzaa uko juu zaidi maeneo ya vijijini kuliko mijini. Kwa wastani, wanawake wa vijijini


huzaa watoto 5.5 katika maisha yao, ikilinganishwa na wanawake wa mijini ambao huzaa watoto 3.6.

**Kiwango cha uwezo wa kuzaa, jumla ya viwango vya uwezo wa kuzaa na kiwango cha uwezo wa kuzaa kwa ujumla, kwa miaka 3 iliyopita kabla ya utafiti, kwa Makazi, Tanzania DHS-MIS 2022**



- TFR: Jumla ya kiwango uzazi kwa kila mwanamke
- GFR: Kiwango cha jumla cha uzazi kwa kila wanawake 1,000 wenye umri wa miaka 15–44
- CBR: Kiwango cha uzazi kwa watu 1,000 kwa kipindi cha mwaka mmoja.

**Kiwango cha jumla cha uwezo wa kuzaa katika kipindi cha miaka 3 kabla ya mwaka wa Utafiti, Tanzania**



## **Mimba za Utotoni**


Mimba za utotoni ni asilimia ya wanawake wenye umri wa miaka 15-19 ambao wamewahi kupata ujauzito kulingana na historia ya mimba iliyotumika katika Utafiti wa TDHS-MIS wa Mwaka 2022. Hii inajumuisha wanawake ambao walijifungua watoto hai, wanawake ambao walipata ujauzito ambao uliishia kwa matokeo mengine tofauti ya kuzaliwa mtoto hai kama vile, kuzaa mtoto mfu, kuharibika kwa mimba, au kutoa mimba na kwa wanawake ambao kwa sasa ni wajawazito kwa mara ya kwanza.

- Asilimia 22 ya wanawake wenye umri wa miaka 15–19 wamewahi kupata ujauzito.
- Asilimia 16 ya wanawake wenye umri wa miaka 15–19 wamewahi kujifungua watoto hai.
- Asilimia 2 ya wanawake wenye umri wa miaka 15–19 walipoteza ujauzito.
- Asilimia 6 ya wanawake wenye umri wa miaka 15–19 walikuwa wajawazito kipindi cha utafiti.

## **Hali ya Lishe ya Mtoto**

- a) Asilimia 30 ya watoto walio na umri chini ya miaka 5 walikuwa na udumavu (wafupi kwa kulinganisha na kigezo cha umri wao) na asilimia 9 ya watoto walikuwa na udumavu mkali.
- b) Asilimia 3 ya watoto walio na umri chini ya miaka 5 walikuwa na ukondefu (wembamba kwa kulinganisha na kigezo cha urefu wao),
- c) Asilimia 4 ya watoto walikuwa na uzito uliozidi
- d) Asilimia 12 ya watoto walio na umri chini ya miaka 5 walikuwa na uzito pungufu, na asilimia 3 ya watoto walikuwa na uzito pungufu sana.


## Asilimia ya Watoto Walio na Umri wa Miaka 5 wenye Utapiamlo



## Vifo vya Utotoni

Viwango vyote vitatu vya vifo vya watoto vimepungua kwa kiasi kikubwa kwa tafiti zote zilizofanyika tangu mwaka 2010. Kwa mfano, kiwango cha vifo vya watoto chini ya miaka 5 kilipungua kutoka vifo 81 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai katika Utafiti wa TDHS wa mwaka 2010 hadi vifo 43 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai katika Utafiti wa TDHS-MIS wa mwaka 2022. Vifo vya watoto wachanga kabla ya kutimiza mwezi mmoja vilipungua kwa kasi ndogo zaidi.

## Mwenendo wa Vifo vya utotoni katika vizazi hai 1,000 katika kipindi cha miaka 5 kabla ya mwaka wa Utafiti



## Utafiti wa Kufuatilia Kaya Tanzania (Awamu ya 5; 2020-2021)

Utafiti wa Kufuatilia Kaya Tanzania (National Panel Survey - NPS) ni utafiti wa ngazi ya kaya wenye uwakilishi wa kitaifa ambao hukusanya taarifa zinazohusiana na hali ya maisha ya watu, ikiwemo matumizi ya bidhaa za chakula na zisizo za chakula katika kaya, uzalishaji katika kilimo na shughuli nyingine za Kipato zisizo za kilimo na takwimu za kiuchumi na kijamii.

Neno “panel” linamaanisha kuwa utafiti utafuatilia kaya na wanakaya walewale kutoka sampuli asili kwa kipindi fulani ili kutambua mabadiliko ya hali zao za maisha.

Utafiti wa NPS ulibuniwa ili kutimiza malengo makuu matatu yafuatayo;

Kwanza, kufuatilia maendeleo ya utekelezaji katika nguzo tatu za uliokuwa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA). Nguzo hizo zilijumuisha: ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato, maisha bora na ustawi wa jamii na utawala bora na uwajibikaji.

Pili, kutoa uelewa mzuri wa viashiria vya kupunguza umaskini. NPS inawezesha utafiti wa kina wa mienendo ya umaskini (kuingia na kutoka kwenye umaskini) katika ngazi ya kitaifa na pia kwa Dar es Salaam, Maeneo Mengine ya Mjini, Vijijini na Zanzibar.

Tatu, kutathmini athari za juhudi za kiseru kwa umma. NPS inaweza kuwa chombo chenye nguvu katika kutathmini matokeo ya sera na programu za maendeleo zinazotekelezwa na serikali pamoja na taasisi zisizo za kiserikali.

### Vifuatavyo ni viashiria muhimu vya Utafiti wa Kufuatilia Kaya Tanzania (NPS) **Kuimarika na Kupungua kwa Ustawi wa Kaya**

- Nchini Tanzania chini ya nusu (42.6%) ya kaya zilizokuwa katika kundi la chini zaidi la matumizi mwaka 2014/15 zilibakia kwenye kundi hilo katika mwaka 2020/21
- Zaidi ya nusu ya kaya zilizokuwa maskini zaidi mwaka 2014/15 ziliweza kuingia katika makundi ya juu ya matumizi.

- Takribani asilimia tatu ya kaya zilizokuwa kundi la chini zaidi la matumizi katika mwaka 2014/15 ziliingia katika kundi la juu zaidi la matumizi mwaka 2020/21.

### Kuingia na Kutoka katika Makundi ya Matumizi (asilimia), Tanzania

NPS 2020/21						
		Kundi la Matumizi/Ustawi wa Kaya				
		Chini zaidi 20%	Chini 20%	Kati 20%	Juu 20%	Juu zaidi 20%
NPS 2014/ 15	Chini zaidi 20%	42.6	23.3	17.6	13.2	3.4
	Chini 20%	27.8	27.3	24.0	14.3	6.6
	Kati 20%	17.2	24.8	24.5	21.3	12.2
	Juu 20%	8.5	17.5	20.6	28.2	25.2
	Juu zaidi 20%	3.7	6.1	12.8	23.6	53.8

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2020-2021 NPS

## Vifupisho, Visawe, Alama na Tanbihi

CBR	Kiwango cha Uzazi
CIF	Gharama za bidhaa, bima na Usafirishaji
COVID	UVIKO
DRC	Jamhuri ya Kidemocratic ya Kongo
EPZ	Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje
FoB	Gharama za bidhaa bila kuhusisha usafirishaji na bima
GDP	Pato la Taifa
JNIA	Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere
KIA	Kiwanja cha Kimataifa cha Kilimanjaro
PHC	Sensa ya Watu na Makazi
PMO	Ofisi ya Waziri Mkuu
TDHS-MIS	Utafiti wa Afya ya Mama na Mtoto na Viashiria vya Malaria
TZS	Tanzanian Shilling
TFR	Kiwango cha Uzazi
TIC	Kituo cha Uwekezaji Tanzania
USD	Dola ya Marekani
VAT	Kodi ya Ongezeko la Thamani
WHO	Shirika la Afya Duniani
NA	Haihusiki
na	Takwimu hazikupatikana
-	Nil/Zero
p	Takwimu za awali
r	Takwimu Zimeboreshwa

Namba/Desimali ya Karibu

Kila tarakimu imeandikwa kwa namba/desimali ya karibu hivyo zikijumlishwa zinaweza zisiwe sawa na jumla





## 1.0 Usuli

Tanganyika ilipata uhuru na kuwa Jamhuri tarehe 9 Disemba mwaka 1961 na 1962 mtawalia. Zanzibar ilipata uhuru tarehe 10 Disemba mwaka 1963 na kuwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar baada ya mapinduzi ya tarehe 12 Januari mwaka 1964. Dola hizi mbili zenye mamlaka ziliungana na kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 26 Aprili 1964.

Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba 2020 ulimuweka madarakani Mh. Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa Rais wa tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha pili cha miaka mitano. Hata hivyo, kufuatia kifo chake cha ghafla mnamo mwezi Machi 2021, Mheshimiwa. Dkt Samia Suluhu Hassan alirithi urais kulingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Rais wa sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Dodoma ni Makao makuu ya nchi na Dar es Salaam ni jiji kuu la kibiashara. Sarafu rasmi ni Shilingi ya Kitanzania (TZS) na lugha ya taifa ni Kiswahili pia Kiingereza kinatumika kama lugha rasmi.

## 2.0 Jiografia

### Mahali ilipo, Mipaka na Eneo

Tanzania ipo Mashariki mwa Afrika kati ya longitudo 29<sup>0</sup> na 41<sup>0</sup> Mashariki, na latitudo 1<sup>0</sup> na 12<sup>0</sup> Kusini:

Ncha ya juu Kaskazini	Mutukula	1 <sup>0</sup> 01'S na 31 <sup>0</sup> 25' E,
Ncha ya chini ya Kusini	Mtalika	11 <sup>0</sup> 32'S na 37 <sup>0</sup> 05' E,
Ncha ya kushoto ya Magharibi	Kigoma	4 <sup>0</sup> 52'S na 29 <sup>0</sup> 38' E
Ncha ya kulia ya Mashariki	Msimbati	10 <sup>0</sup> 21'S na 40 <sup>0</sup> 26' E.

Tanzania Bara inapakana na nchi/bahari zifuatazo:

Kaskazini:	Kenya na Uganda.
Magharibi:	Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.
Kusini Magharibi:	Zambia na Malawi.
Kusini:	Msumbiji.
Mashariki:	Bahari ya Hindi.

Tanzania Zanzibar ipo katika Bahari ya Hindi umbali wa kilomita zipatazo 30 kutoka Tanzania Bara.

### Eneo la Mraba la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 2022

Mahali	("000" Km za Mraba.)
<b>Tanzania (jumla ya eneo)</b>	<b>945.5</b>
Eneo la maji	61.5
Eneo la ardhi	884.0
Tanzania Bara	881.3
Tanzania Zanzibar	2.7

**Visiwa Vikuu Tanzania Bara (km za mraba).**

Ukerewe .....	647.0
Mafia .....	518.0

**Visiwa Vikuu Tanzania Zanzibar (Km za Mraba).**

Unguja .....	1,666.0
Pemba .....	988.0

**Eneo la Maji**

**Tanzania Bara ("000" Km za mraba.)**

**Maziwa Makuu:**

Victoria	34.9
Tanganyika	13.4
Nyasa	5.6
Rukwa	2.8
Eyasi	1.0

**Maeneo mengine ya maji (mabwawa, mito) 3.8**

**Jumla 61.5**

## Vilele vya Milima, Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba

### Baadhi ya Vilele vya Milima Kwa Mkoa na Urefu (mita), Tanzania, 2022

Na.	Jina	Mkoa	Mita juu ya Usawa wa Bahari
1	Kilimanjaro	Kilimanjaro	5,895
2	Meru	Arusha	4,566
3	Klute	Kilimanjaro	3,952
4	Lool Malasin	Kilimanjaro	3,648
5	Shira	Kilimanjaro	3,626
6	Oldeani	Manyara/Arusha	3,188
7	Hanang	Manyara	3,103
8	Jaeger	Arusha	3,050
9	Monduli	Arusha	3,000
10	Mtorwi	Iringa	2,961
11	Rungwe	Mbeya	2,960
12	Chaluhangi	Mbeya	2,933
13	Kitumbeine	Arusha	2,858
14	Mbeya	Mbeya	2,826
15	Salala	Iringa	2,688
16	Uluguru	Morogoro	2,648
17	Kimhondu	Morogoro	2,646
18	Longido	Arusha	2,629
19	Ngozi	Mbeya	2,620
20	Rubeho	Morogoro	2,576
21	Luhombero	Iringa	2,576
22	Olosha	Arusha	2,526
23	Likongowele	Lindi	2,524
24	Livingstone	Mbeya/Njombe	2,521
25	Shengena	Kilimanjaro	2,462

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

## Hifadhi za Taifa kwa Eneo la Mraba na Wilaya (Mkoa), Tanzania, 2022

Na.	Jina	Wilaya (Mkoa)	Eneo (Km2)
1	Nyerere	Kisarawe na Rufiji (Pwani), Morogoro Vijijini, Kilombero, Ulanga, (Morogoro), Tunduru and Namtumbo (Ruvuma), Liwale (Lindi)	30,893
2	Ruaha	Iringa Vijijini na Mufindi (Iringa); Mbarali na Chunya (Mbeya); Chamwino (Dodoma)	20,300
3	Serengeti	Meatu, Itilima, Busega na Bariadi (Simiyu); Bunda, Serengeti na Tarime (Mara); Ngorongoro (Arusha)	14,763
4	Kigosi	Biharamulo (Kagera), Bukombe na Mbogwe (Geita), Kaliua (Tabora) na Ushetu (Shinyanga)	7,460
5	Burigi-Chato	Biharamulo, Muleba, Ngara, Karagwe (Kagera) na Chato (Geita)	4,707
6	Katavi	Mpanda, Mlele, Nkasi na Tanganyika (Katavi)	4,471
7	Ugalla River	Urambo na Kaliua (Tabora)	3,865
8	Mkomazi	Same na Mwanga (Kilimanjaro); Lushoto, Korogwe na Mkinga (Tanga)	3,245
9	Mikumi	Kilosa, Morogoro na Mvomero (Morogoro)	3,245
10	Tarangire	Babati, Kiteto na Simanjiro (Manyara); Monduli (Arusha); Kondoa (Dodoma)	2,600
11	Udzungwa	Kilombero na Kilosa (Morogoro); Kilolo (Iringa)	1,990

<b>Na.</b>	<b>Jina</b>	<b>Wilaya (Mkoa)</b>	<b>Eneo (Km2)</b>
12	Kilimanjaro	Siha, Hai, Rombo na Moshi Vijijini (Kilimanjaro); Longido (Arusha)	1,668
13	Mahale	Uvinza (Kigoma)	1,613
14	Saadani	Bagamoyo (Pwani); Pangani na Handeni (Tanga)	1,100
15	Lake Manyara	Babati na Mbulu (Manyara); Karatu na Monduli (Arusha)	648.7
16	Arusha	Arumeru na Longido (Arusha)	552
17	Kitulo	Makete (Njombe), Mbeya Vijijini na Rungwe (Mbeya)	465
18	Rubondo	Muleba (Kagera); Sengerema (Mwanza); Geita na Chato (Geita)	457
19	Ibanda-Kyerwa	Kyerwa (Kagera)	298.6
20	Rumanyika-Karaawe	Kyerwa (Kagera)	247
21	Gombe Stream	Kigoma Mjini (Kigoma)	71
22	Saanane Island	Nyamagana, Sengerema na Ilemela (Mwanza)	2.18
<b>Jumla ya Eneo</b>			<b>104,661,48</b>

*Chanzo: Wizara Maliasili na Utalii*

**Mapori ya Akiba, Tanzania, 2022**

<b>Na.</b>	<b>Jina</b>	<b>Mkoa</b>	<b>Ukubwa (Km2)</b>
1	Selous	Lindi na Ruvuma	18,020.00
2	Rungwa	Singida na Mbeya	9,000.00
3	Ugalla	Tabora	7,577.36
4	Kilombero	Morogoro	6,989.30
5	Inyonga	Katavi	6,569.93
6	Moyowosi	Kigoma	6,000.00
7	Luganzo Tongwe	Katavi, Tabora na Kigoma	5,746.16
8	Wembere	Tabora na Singida	5,385.81
9	Uwanda	Rukwa	5,000.00
10	Kizigo	Singida	4,000.00
11	Rukwa	Katavi	4,000.00
12	Lukwati	Songwe	3,146.00
13	Ikorongo	Mara	3,000.00
14	Piti	Songwe	2,972.93
15	Wami Mbiki	Morogoro na Pwani	2,466.58
16	Lwafi	Rukwa	2,228.00
17	Maswa	Simiyu	2,200.00
18	Grumeti	Mara	2,000.00
19	Muhesi	Singida	2,000.00
20	Mpanga-Kipengere	Njombe na Mbeya	1,574.25
21	Igombe	Tabora	1,367.14
22	Swagaswaga	Dodoma na Singida	871
23	Mkungunero	Dodoma na Manyara	743.9
24	Liparamba	Ruvuma	570
25	Lukwika-Lumesule	Mtwara	444
26	Msanjesi	Mtwara	210
27	Kijereshi	Simiyu	82
28	Pande	Dar es salaam	12
<b>Jumla</b>			<b>104,176.36</b>

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

## Viwango vya Mvua na Joto

### Kiwango cha Mvua (mm) kwa Mwezi kwa Baadhi ya Vituo vya Hali ya Hewa, Tanzania, 2022

Kituo	Jan	Feb	Mac	Apr	Mei	Jun	Jul	Ago	Sep	Okt	Nov	Des	Mwaka
Dodoma	116.1	232.6	186.6	1.2	1.1	0.1	0.0	0.0	0.0	0.0	32.6	116.6	686.9
Arusha	62.1	135.3	90.9	97.8	5.9	26.5	3.4	0.0	0.6	0.0	64.4	95.4	582.3
Kilimanjaro	96.1	13.8	45.5	6.2	6.4	1.0	0.0	1.3	0.0	2.7	173.0	96.1	442.1
Tanga	35.8	61.6	72.3	116.2	56.9	92.0	115.3	24.0	68.0	135.2	121.2	135.3	1,033.8
Morogoro	116.1	232.6	186.6	1.2	1.1	0.1	0.0	0.0	0.0	0.0	32.6	116.6	686.9
Kibaha	108.6	147.1	78.2	156.3	48.7	2.8	27.0	11.5	1.8	4.3	45.2	52.4	683.9
Dar es Salaam	74.6	56.5	109.2	124.8	56.4	2.9	44.6	10.1	21.8	5.7	85.9	79.0	671.5
Kilwa Masoko	182.3	208.7	151.3	242.6	5.3	0.0	12.9	0.5	5.6	0.0	4.5	69.1	882.8
Mtwara	123.2	197.1	120.5	154.1	5.1	30.2	3.7	11.8	13.5	0.2	3.0	75.0	737.4
Songea	340.8	377.5	289.4	290.8	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	52.1	247.6	1,598.2
Bukoba	89.6	178.3	227.9	391.5	240.6	69.6	11.4	57.6	103.6	122.9	179.1	257.6	1,929.7
Musoma	111.6	93.7	51.1	219.8	188.4	19.0	0.0	68.2	70.9	34.0	102.8	79.0	1,038.5
Mwanza	167.4	141.1	129.9	107.3	126.1	40.6	0.0	76.7	0.0	12.7	125.1	146.0	1,072.9
Shinyanga	45.9	169.1	48.5	77.7	15.8	0.0	0.0	1.0	0.0	4.8	182.7	174.0	719.5
Kigoma	119.9	46.3	138.3	80.1	100.8	0.0	0.9	0.0	7.9	46.4	98.9	191.2	830.7
Singida	122.1	258.4	142.7	21.5	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	22.9	170.6	738.2
Tabora	204.4	161.1	60.2	67.2	1.1	0.0	0.0	0.0	6.4	26.0	117.2	139.3	782.9
Sumbawanga	87.1	155.0	170.9	66.7	10.6	0.0	0.0	0.0	0.0	82.2	0.0	151.4	723.9
Iringa	214.7	110.6	126.4	67.1	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	24.1	210.9	753.8
Songwe	277.1	295.5	135.0	56.7	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	82.4	221.3	1,068.0
Same	46.8	68.6	24.3	55.3	2.1	1.7	1.3	0.0	2.4	4.8	0.0	42.6	249.9
Karume (pemba)	52.6	36.0	46.1	427.4	110.6	111.6	73.5	22.0	14.8	92.9	32.8	9.1	1,029.4
Mpanda	201.3	80.6	268.8	65.8	8.1	0.0	0.0	0.7	0.0	0.0	185.8	230.8	1,041.9
Ilonga	305.6	279.6	54.1	60.7	11.8	1.4	4.5	6.1	0.0	0.8	55.9	53.7	834.2
Zanzibar	241.2	63.9	62.6	318.4	42.0	9.6	75.5	38.0	7.7	9.7	189.3	212.4	1,270.3
Mahenge	282.3	210.0	157.4	129.8	14.7	0.8	8.2	3.5	0.3	2.6	19.3	135.2	963.8

Chanzo: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania



**Kiwango vya Mvua (mm) kwa Mwaka kwa Baadhi ya Vituo vya Hali ya Hewa, Tanzania, 2018 – 2022**

<b>Kituo</b>	<b>2018</b>	<b>2019</b>	<b>2020</b>	<b>2021</b>	<b>2022</b>	<b>Wastani</b>
Bukoba	1,706.9	2,701.8	2,054.0	2,245.2	1,929.7	2,127.5
Mahenge	1,728.0	2,205.9	2,320.0	1,279.5	963.8	1,699.4
Mtwara	1,180.7	1,084.4	1,168.8	1,435.9	737.4	1,121.4
Tanga	1,333.9	1,644.9	1,165.1	964.5	1,033.8	1,228.4
Songea	1,039.0	1,234.7	1,564.4	901.5	1,598.2	1,267.6
Dar es Salaam	1,208.4	1,666.7	1,826.8	971.3	671.5	1,268.9
Mwanza	1,153.0	1,154.0	1,148.2	1,226.7	1,072.9	1,151.0
Musoma	1,031.0	1,239.6	1,236.5	1,000.7	1,038.5	1,109.3
Ilonga	911.1	1,424.2	1,303.0	776.9	834.2	1,049.9
Tabora	1,112.9	966.5	1,360.6	649.9	782.9	974.6
Kigoma	985.1	758.2	955.1	1,103.2	830.7	926.5
Songwe	1,042.8	880.7	974.4	944.1	1,068.0	982.0
Mpanda	1,091.2	1,363.3	1,492.5	1,010.1	1,041.9	1,199.8
Arusha	1,197.9	1,236.5	1,160.7	720.5	582.3	979.6
Sumbawanga	768.4	899.5	1,110.8	563.9	723.9	813.3
Singida	763.4	839.9	1,041.3	623.6	738.2	801.3
Iringa	509.3	725.6	1,201.6	441.9	753.8	726.4
Dodoma	679.3	770.5	1,116.6	598.1	686.9	770.3
Same	626.1	969.7	469.1	418.6	249.9	546.7
Kilimanjaro	861.8	626.2	807.7	394.3	442.1	626.4

Chanzo: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania  
"na" –Taarifa haikutikana

**Wastani wa Kiwango cha Juu cha Joto (°C) kwa Mwaka kwa Baadhi ya Vituo vya Hali ya Hewa Tanzania, 2018 – 2022**

<b>Kituo</b>	<b>2018</b>	<b>2019</b>	<b>2020</b>	<b>2021</b>	<b>2022</b>	<b>Wastani</b>
Bukoba	26.4	26.9	26.8	26.5	26.3	26.6
Mwanza	28.4	29.2	27.9	29.0	28.7	28.6
Musoma	na	29.0	29.0	29.2	28.7	29.0
Kigoma	29.4	29.8	29.1	29.8	28.9	29.4
Sumbawanga	24.8	25.2	26.7	25.9	24.8	25.5
Tabora	28.4	30.4	29.6	30.1	30.0	29.7
Singida	26.0	27.1	26.8	27.3	27.1	26.9
Dodoma	28.7	29.5	28.9	29.1	26.5	28.5
Iringa	26.4	27.2	26.8	27.2	28.8	27.3
Same	29.2	29.6	29.3	30.0	29.9	29.6
Arusha	25.4	26.3	25.8	26.0	26.1	25.9
Kilimanjaro	29.4	30.4	29.6	30.2	30.5	30.0
Tanga	30.8	31.6	31.5	31.2	30.8	31.2
Dar es Salaam	31.5	29.2	31.5	na	31.4	30.9
Mtwara	31.1	31.2	31.0	30.9	30.8	31.0
Songea	na	27.5	27.7	28.2	27.4	27.7
Mahenge	24.9	24.9	na	na	25.2	25.0
Songwe	28.1	28.7	28.0	28.0	27.7	28.1

Chanzo: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

Tanbihi: 'na' –Taarifa haikupatikana

**Wastani wa Kiwango cha Juu cha Joto (°C) kwa Mwezi kwa Baadhi ya Vituo vya Hali ya Hewa, Tanzania, 2022**

Kituo	Jan	Feb	Mac	Apr	Mei	Jun	Jul	Ago	Sep	Okt	Nov	Des	Mwaka
Dodoma	30.8	27.2	29.6	29.8	28.3	26.5	25.9	27.2	28.5	30.0	31.3	30.4	28.8
Arusha	28.6	26.8	29.1	26.5	24.9	22.4	22.7	23.7	25.3	27.6	27.5	28.2	26.1
Kilimanjaro	33.5	31.4	34.1	31.6	29.7	26.6	26.6	27.4	28.9	31.1	32.2	32.9	30.5
Tanga	32.2	32.4	33.1	31.8	31.0	29.8	28.2	28.3	29.2	29.9	31.6	32.0	30.8
Morogoro	30.8	27.2	29.6	29.8	28.3	26.5	25.9	27.2	28.5	30.0	31.3	30.4	28.8
Kibaha	32.0	31.8	33.8	32.3	31.4	30.8	29.1	29.8	31.7	31.3	32.9	32.5	31.6
Dar es Salaam	32.3	32.2	33.3	31.7	31.4	30.6	28.7	29.9	30.8	31.4	32.5	32.3	31.4
Kilwa Masoko	32.2	31.6	31.6	31.4	30.9	29.5	28.5	28.4	28.8	29.2	30.6	31.7	30.4
Mtwara	31.7	30.9	31.6	31.7	31.3	30.0	29.4	29.8	30.2	30.4	31.4	31.7	30.8
Songea	29.3	28.5	28.3	28.0	26.9	24.4	23.6	24.9	26.8	29.3	30.4	27.9	27.4
Bukoba	26.5	25.6	26.7	26.6	26.2	26.2	26.3	26.3	26.5	27.2	26.1	25.5	26.3
Musoma	29.3	28.6	30.0	29.7	28.7	29.0	29.3	28.1	27.9	29.1	27.7	27.2	28.7
Mwanza	28.6	27.5	29.5	29.2	29.4	28.9	29.8	28.7	28.7	30.4	27.4	26.7	28.7
Shinyanga	29.8	26.9	30.5	30.6	30.3	29.8	30.0	31.0	32.2	33.7	30.9	28.5	30.4
Kigoma	28.7	27.7	28.8	28.4	28.4	28.4	29.0	29.8	31.1	31.3	27.6	27.6	28.9
Singida	27.2	25.1	28.0	27.7	26.9	25.4	24.8	26.3	28.1	29.3	29.1	27.3	27.1
Tabora	28.9	26.9	29.7	30.1	29.8	29.3	29.3	30.6	32.3	33.3	31.1	29.1	30.0
Sumbawanga	24.6	23.5	24.8	25.7	25.0	24.2	23.2	25.3	26.0	27.7	25.0	23.0	24.8
Iringa	27.0	24.8	27.1	26.9	26.2	24.6	23.6	25.5	26.8	29.0	29.3	27.5	26.5
Mbeya	17.7	16.9	17.4	17.1	16.2	14.7	14.4	14.8	16.0	17.6	17.5	17.2	16.5
Same	31.9	31.7	33.7	31.1	29.2	27.2	26.3	26.9	27.8	30.3	31.0	31.8	29.9
Karume (Pemba)	31.5	32.0	31.8	30.6	29.8	28.3	27.2	27.5	28.1	28.7	30.4	31.7	29.8
Mpanda	28.0	28.1	29.7	29.9	29.8	29.1	29.4	31.3	32.8	34.6	29.6	27.4	30.0
Ilonga	32.6	30.0	31.6	31.1	31.2	28.5	27.4	27.4	30.4	32.0	34.0	33.7	30.8
Zanzibar	32.7	32.3	33.5	31.1	31.2	30.4	28.7	29.1	30.4	30.9	31.1	32.0	31.1
Mahenge	26.5	26.3	26.1	25.0	23.8	22.7	22.5	23.7	24.2	25.8	28.2	27.1	25.2

Chanzo: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

**Wastani wa Kiwango cha Chini cha Joto (°C) kwa Mwaka kwa Baadhi ya Vituo vya Hali ya Hewa, Tanzania, 2018 – 2022**

<b>Kituo</b>	<b>2018</b>	<b>2019</b>	<b>2020</b>	<b>2021</b>	<b>2022</b>	<b>Wastani</b>
Bukoba	18.6	18.7	19.0	26.5	18.3	20.2
Mwanza	18.6	18.7	18.6	29.0	18.2	20.6
Musoma	19.1	19.8	19.4	29.2	19.3	21.4
Kigoma	19.1	19.6	19.6	29.8	19.4	21.5
Tabora	17.4	17.4	17.3	30.1	16.9	19.8
Singida	16.2	16.7	17.5	27.3	15.8	18.7
Dodoma	17.7	18.3	18.0	29.1	17.8	20.2
Iringa	15.6	16.2	15.7	27.2	15.1	18.0
Same	18.6	19.2	19.0	29.8	18.9	21.1
Arusha	15.5	15.8	15.8	26.0	15.4	17.7
Kilimanjaro	17.9	20.2	18.6	30.2	18.8	21.1
Tanga	23.1	25.1	na	31.2	23.2	25.7
Dar es Salaam	22.4	23.3	23.0	na	22.6	22.8
Mtwara	21.5	22.0	22.1	30.5	21.5	23.5
Songea	14.9	16.9	17.2	28.2	16.6	18.8
Mahenge	17.3	17.8	18.2	na	17.4	17.7
Songwe	16.7	16.9	16.9	16.7	16.5	16.7

Chanzo: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

'na' – Taarifa haikupatikana

## Wastani wa Kiwango cha Chini cha Joto (°C) kwa Mwezi kwa Baadhi ya Vituo vya Hali ya Hewa, Tanzania, 2022

Kituo	Jan	Feb	Mac	Apr	Mei	Jun	Jul	Ago	Sep	Okt	Nov	Des	Mwaka
Dodoma	20.1	19.0	19.7	19.2	17.3	16.0	14.9	15.4	16.0	16.7	19.3	19.7	17.8
Arusha	15.0	16.5	16.0	17.2	16.7	14.7	14.2	14.0	14.0	14.4	16.6	15.7	15.4
Kilimanjaro	19.2	20.0	20.3	20.6	19.6	17.7	17.1	16.7	16.6	17.5	20.0	19.7	18.8
Tanga	24.3	24.8	24.9	24.9	23.8	22.3	21.3	20.8	21.6	22.0	23.8	24.4	23.2
Morogoro	22.4	22.0	22.3	21.4	19.1	16.9	16.8	16.7	17.3	18.0	20.6	21.8	19.6
Kibaha	23.9	23.6	23.9	23.2	22.1	20.8	19.9	19.8	20.6	21.0	23.7	24.0	22.2
Dar es Salaam	25.6	25.2	25.2	23.9	22.5	20.9	19.8	19.3	20.4	20.4	23.6	24.8	22.6
Kilwa Masoko	25.6	24.3	25.1	24.5	23.7	21.6	21.2	21.4	22.4	23.5	25.9	25.6	23.7
Mtwara	24.0	23.2	23.4	22.5	21.7	20.3	19.4	18.7	19.8	19.2	22.2	23.4	21.5
Songea	19.3	19.0	18.7	18.2	14.7	12.8	12.3	13.9	15.0	16.7	19.3	19.3	16.6
Bukoba	18.3	17.8	18.1	18.5	18.4	18.1	18.2	18.7	18.1	18.6	19.0	17.9	18.3
Musoma	19.5	19.4	20.5	19.5	19.4	18.6	18.0	18.6	19.0	19.6	19.7	19.5	19.3
Mwanza	18.8	18.9	18.9	19.2	18.5	16.6	16.3	16.9	19.7	18.1	18.8	17.9	18.2
Shinyanga	19.1	18.4	19.2	18.8	18.5	16.7	15.9	17.8	19.3	20.2	19.9	19.2	18.6
Kigoma	20.3	20.4	20.2	20.2	19.5	17.2	16.6	18.2	19.7	20.2	20.3	19.7	19.4
Singida	17.1	16.6	17.3	17.2	16.0	14.2	13.4	14.1	15.0	15.5	16.4	17.3	15.8
Tabora	15.8	15.0	17.0	16.6	16.0	14.8	15.2	17.0	18.3	19.5	19.1	18.6	16.9
Sumbawanga	14.5	14.2	14.4	14.8	12.9	10.6	10.6	11.3	13.3	15.3	16.3	15.2	13.6
Iringa	17.4	17.2	16.9	15.9	14.7	13.5	12.7	12.8	13.3	13.4	15.9	17.0	15.1
Mbeya	17.7	16.9	17.4	17.1	16.2	14.7	14.4	14.8	16.0	17.6	17.5	17.2	16.5
Same	20.7	20.5	20.7	20.5	19.0	17.4	16.4	16.3	16.8	17.6	20.1	20.8	18.9
Karume (Pemba)	24.7	25.0	25.6	24.1	22.9	21.9	22.5	23.2	24.0	25.1	24.7	25.0	24.1
Mpanda	20.0	19.3	19.3	19.2	16.9	13.9	12.8	14.9	17.7	19.3	19.7	19.0	17.7
Ilonga	22.0	21.8	22.0	21.5	19.8	17.1	16.5	17.8	19.1	20.5	21.8	22.2	20.2
Zanzibar	25.5	25.5	25.7	25.1	25.1	23.8	22.2	21.4	20.9	22.6	24.2	24.8	23.9
Mahenge	19.3	19.3	18.9	19.0	17.3	15.7	14.9	15.2	15.7	16.0	18.5	19.2	17.4

Chanzo: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

### 3.0 Siasa

#### Idadi ya Majimbo Kimkoa, Tanzania, Desemba 2022



Chanzo: Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC)

## Vyama vyenye Usajili wa Kudumu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Desemba 2022

Na.	Jina la Chama	Jina kwa Kifupi	Mwaka Kilipoanzishwa
1.	Chama cha Mapinduzi	CCM	01 Julai, 1992 (Kilianzishwa 1977)
2.	Civil United Front (Chama cha Wananchi)	CUF	21 Januari, 1993
3.	Chama cha Demokrasia na Maendeleo	CHADEMA	21 Januari, 1993
4.	Union for Multiparty Democracy	UMD	21 Januari, 1993
5.	National Convention for Construction and Reform	NCCR-MAGEUZI	21 Januari, 1993
6.	National League for Democracy	NLD	21 Januari, 1993
7.	United People's Democratic Party	UPDP	04 Februari, 1993
8.	National Reconstruction Alliance	NRA	08 Februari, 1993
9.	Tanzania Democratic Alliance	ADA-TADEA	05 Aprili, 1993
10.	Tanzania Labour Party	TLP	24 Novemba, 1993
11.	United Democratic Party	UDP	24 Machi, 1994
12.	Demokrasia Makini	MAKINI	15 Novemba, 2001
13.	Democratic Party	DP	07 Juni, 2002
14.	Sauti ya Umma	SAU	17 Februari, 2005
15.	Alliance for Tanzania Farmers Party	AFP	03 Novemba, 2009
16.	Chama cha Kijamii	CCK	27 Januari, 2012
17.	Alliance for Democratic Change	ADC	28 Agosti, 2012
18.	Chama cha Ukombozi wa Umma	CHAUMA	04 Juni, 2013
19.	Alliance for Change and Transparency	ACT-WAZALENDO	05 Mei, 2014

Chanzo: Ofisi ya Msajili Mkuu wa Vyama vya Siasa

## Matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020

Uchaguzi wa Rais: Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Oktoba, 2020

Na.	Jina la Mgombea	Jina la Chama cha Siasa	Idadi ya Kura Alizopata	Asilimia kwa Kura Halali Zilizopigwa
1	Dkt. John Pombe Joseph Magufuli	CCM	12,516,252	84.40
2	Mahona Leopold Lucas	NRA	80,787	0.54
3	Shibuda John Paul	ADA TADEA	33,086	0.22
4	Muttamwega Bhatt Mgaywa	SAU	14,922	0.10
5	Cecilia Augustino Mmanga	DEMOKRASIA MAKINI	14,556	0.10
6	Maganja Yerima Kulwa	NCCR MAGEUZI	19,969	0.13
7	Lipumba Ibrahim Haruna	CUF	72,885	0.49
8	Philipo John Fumbo	DP	8,283	0.06
9	Membe Bernard Kamilius	ACT-WAZALENDO	81,129	0.55
10	Queen Cuthbert Sendiga	ADC	7,627	0.05
11	Twalid Ibrahim Kadege	UPDP	6,194	0.04
12	Rungwe Hashim Spunda	CHAUMA	32,878	0.22
13	Mazrui Khalfani Mohamed	UMD	3,721	0.03
14	Seif Maalim Seif	AFP	4,635	0.03
15	Lissu Tundu Antiphias Mughwai	CHADEMA	1,933,271	13.04
<b>Jumla</b>			<b>14,830,195</b>	<b>100.00</b>

Chanzo: Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC)



**Uchaguzi wa Rais: Tanzania Zanzibar, Oktoba, 2020**

<b>Na.</b>	<b>Jina la Mgombea</b>	<b>Jina la Chama</b>	<b>Idadi ya Kura Alizopata</b>	<b>Asilimia kwa Kura Zilizopigwa</b>
1	Dkt. Hussein Ali Mwinyi	CCM	380,402	76.27
2	Seif Sharif Hamad	ACT- WAZALENDO	99,103	19.87
3	Said Soud Said	AFP	285	0.06
4	Juma Ally Khatib	ADA TADEA	392	0.08
5	Hamad Rashid Mohammed	ADC	996	0.20
6	Othman Rashid Khamis	CCK	2,235	0.45
7	Said Issa Mohammed	CHADEMA	1,702	0.34
8	Ally Omar Juma	CHAUMMA	249	0.05
9	Mussa Haji Kombo	CUF	1,428	0.29
10	Shafi Hassan Suleim	DP	106	0.02
11	Amour Hassan Amour	DEMOKRASIA MAKINI	133	0.03
12	Mfaume Khamis Hassan	NLD	122	0.02
13	Khamis Fakhi Mgau	NRA	160	0.03
14	Issa Mohamed Zonga	SAU	102	0.02
15	Mwalimu Hussein Juma	TLP	142	0.03
16	Mohamed Omar Suleiman	UMD	104	0.02
17	Hamad Mohamed Ibrahim	UPDP	181	0.04
<b>Jumla</b>			<b>498,786</b>	<b>100.00</b>

*Chanzo: Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC)*

**Wabunge (Idadi) wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Chama/ Madaraka na Jinsi, Desemba, 2022**

Aina ya Uanachama	CCM		CHADEMA		CUF		ACT-WAZALENDO		Wanao ingia kwa Wadhifa wao		Jumla
	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke	
Kuchaguliwa	232	24	0	1	1	2	4	0	-	-	264
Viti Maalumu Wanawake	-	94	-	19	-	0	-	0	-	-	113
Kuteuliwa na Rais	5	5	-	-	-	-	-	-	-	-	10
Kuteuliwa na Baraza la Wawakilishi - Zanzibar	3	2	-	-	-	-	-	-	-	-	5
Mwanasheria Mkuu	-	-	-	-	-	-	-	-	1	-	1
<b>Jumla</b>	<b>240</b>	<b>125</b>	<b>0</b>	<b>20</b>	<b>1</b>	<b>2</b>	<b>4</b>	<b>0</b>	<b>1</b>	<b>-</b>	<b>393</b>

*Chanzo: Ofisi ya Bunge la Tanzania*

**Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi (idadi) kwa Chama/Madaraka na Jinsi, Tanzania Zanzibar, Desemba 2022**

Aina ya Uanachama	CCM		ACT-WAZALENDO		TADEA		Wanao ingia kwa Wadhifa		Jumla
	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke	
Kuchaguliwa	38	8	4	0	0	0	-	-	50
Viti Maalumu Wanawake	-	18	-	0	-	0	-	-	18
Kuteuliwa na Rais	1	3	2	0	1	0	-	-	7
Mwanasheria Mkuu	-	-	-	-	-	-	1	-	1
Spika	1	0	0	0	0	0	-	-	1
<b>Jumla</b>	<b>40</b>	<b>29</b>	<b>6</b>	<b>0</b>	<b>1</b>	<b>0</b>	<b>1</b>	<b>0</b>	<b>77</b>

*Chanzo: Ofisi ya Baraza la Wawakilishi*

**Idadi ya Madiwani kwa Chama cha Siasa, Tanzania Bara, Desemba 2022**

<b>Jina</b>	<b>Idadi</b>
CCM	3,821
CHADEMA	85
ACT-MZALENDO	21
CUF	20
NCCR-MAGEUZI	5
DP	1
<b>Jumla</b>	<b>3,953</b>

*Chanzo: Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC)*

**Idadi ya Madiwani kwa Namna Walivyochaguliwa/Kuteuliwa, Tanzania Zanzibar, Desemba 2022**


<b>Namna ya kuchaguliwa/kuteuliwa</b>	<b>Me</b>	<b>Ke</b>	<b>Jumla</b>
Kuchaguliwa	83	27	110
Kuteuliwa na Waziri	30	25	55
Viti Maalum Wanawake	-	45	45
<b>Jumla</b>	<b>113</b>	<b>97</b>	<b>210</b>

*Chanzo: Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC)*

## 4.0 Idadi ya Watu

Kati ya mwaka 1967 na 2022, idadi ya watu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeongezeka kwa takribani mara tano (5) kutoka milioni 12.3 hadi milioni 61.7. Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, inaonesha wastani wa asilimia 3.2 wa kasi ya ongezeko la idadi ya watu kwa mwaka.

**Mwenendo wa Ongezeko la Idadi ya Watu (Milioni), Tanzania, 1967 – 2022**



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu; Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 1967, 1978, 1988, 2002, 2012 and 2022, Tanzania

**Mgawanyo wa Idadi ya Watu na Wastani wa Kasi ya Ongezeko la Watu kwa Mwaka kwa Mkoa, Tanzania, 2002, 2012 na 2022**


Mkoa	Idadi ya Watu			Asilimia ya ongezeko la watu (2022)
	Sensa ya mwaka 2002	Sensa ya mwaka 2012	Sensa ya mwaka 2022	
<b>Tanzania</b>	<b>34,443,603</b>	<b>44,928,923</b>	<b>61,741,120</b>	<b>3.2</b>
<b>Tanzania Bara</b>	<b>33,461,849</b>	<b>43,625,354</b>	<b>59,851,347</b>	<b>3.2</b>
Dodoma	1,692,025	2,083,588	3,085,625	3.9
Arusha	1,288,088	1,694,310	2,356,255	3.3
Kilimanjaro	1,376,702	1,640,087	1,861,934	1.3
Tanga	1,636,280	2,045,205	2,615,597	2.5
Morogoro	1,753,362	2,218,492	3,197,104	3.7
Pwani	885,017	1,098,668	2,024,947	6.1
Dar es Salaam	2,487,288	4,364,541	5,383,728	2.1
Lindi	787,624	864,652	1,194,028	3.2
Mtwara	1,124,481	1,270,854	1,634,947	2.5
Ruvuma	1,113,715	1,376,891	1,848,794	2.9
Iringa	840,404	941,238	1,192,728	2.4
Mbeya	1,339,848	1,708,548	2,343,754	3.2
Singida	1,086,748	1,370,637	2,008,058	3.8
Tabora	1,710,465	2,291,623	3,391,679	3.9
Rukwa	729,060	1,004,539	1,540,519	4.3
Kigoma	1,674,047	2,127,930	2,470,967	1.5
Shinyanga	1,249,226	1,534,808	2,241,299	3.8
Kagera	1,791,451	2,458,023	2,989,299	2.0
Mwanza	2,058,866	2,772,509	3,699,872	2.9
Mara	1,363,397	1,743,830	2,372,015	3.1
Manyara	1,037,605	1,425,131	1,892,502	2.8
Njombe	648,464	702,097	889,946	2.4
Katavi	408,609	564,604	1,152,958	7.1
Simiyu	1,317,879	1,584,157	2,140,497	3.0
Geita	1,337,718	1,739,530	2,977,608	5.4
Songwe	723,480	998,862	1,344,687	3.0
<b>Tanzania Zanzibar</b>	<b>981,754</b>	<b>1,303,569</b>	<b>1,889,773</b>	<b>3.7</b>
Kaskazini Unguja	136,639	187,455	257,290	3.2
Kusini Unguja	94,244	115,588	195,873	5.3
Mjini Magharibi	390,074	593,678	893,169	4.1
Kaskazini Pemba	185,326	211,732	272,091	2.5
Kusini Pemba	175,471	195,116	271,350	3.3

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu; Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2002, 2012 na 2022

## Kasi ya Ongezeko la Watu kwa Mwaka

Wastani wa kasi ya ongezeko la idadi ya watu kwa mikoa ni kati ya asilimia 1.3 mkoani Kilimanjaro na asilimia 7.1 mkoani Katavi.


### Kasi ya Ongezeko la Watu kwa Mwaka kwa Mkoa, Tanzania, 2022



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu; Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Tanzania

## Piramidi ya Idadi ya Watu

Mgawanyo wa Asilimia ya Idadi ya Watu Wote kwa Umri na Jinsi, Tanzania, Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022



## Viashiria Muhimu vya Sensa za Watu na Makazi za Mwaka 2002, 2012 na 2022, Tanzania

Kiashiria	2002			2012			2022		
	Tanzania	Bara	Zanzibar	Tanzania	Bara	Zanzibar	Tanzania	Bara	Zanzibar
Jumla ya Idadi ya watu (milioni)	34.4	33.5	1.0	44.9	43.6	1.3	61.7	59.8	1.9
Asilimia ya watoto chini ya miaka 15 (miaka 0 na 14)	44.2	44.2	44.3	43.9	43.9	42.5	42.8	42.8	40.8
Uwiano wa Kijinsia (wanaume kwa kila wanawake 100)	96	96	96	95	95	94	95	95	94
Kiwango cha Ukuaji wa kila Mwaka	2.9	2.9	3.1	2.7	2.7	2.8	3.2	3.2	3.7
Asilimia ya Watoto chini ya Miaka 5 (miaka 0 hadi 4)	16.4	16.5	15.7	16.2	16.2	15.6	15.4	15.4	14.6
Asilimia ya Vjana wenye Umri wa 15 hadi 24	19.6	19.6	20.0	19.1	19.0	20.3	19.2	19.2	20.4
Asilimia ya Vjana wenye Umri wa 15 hadi 35	35.6	35.6	36.2	34.7	34.6	36.2	34.5	34.4	37.0
Asilimia ya Watu wenye Umri wa kufanya kazi (miaka 15-64)	51.9	51.8	52.7	52.2	52.5	54.7	53.4	53.4	56.3
Asilimia ya Watu wenye Umri wa Miaka 60 na Zaidi	5.7	5.7	4.6	5.6	5.6	4.5	5.7	5.7	4.5
Asilimia ya Watu wenye Umri wa Miaka 65 na Zaidi	3.9	3.9	3.0	3.9	3.9	2.8	3.8	3.8	2.9
Asilimia ya Idadi ya Watu wa Mjini	23.1	22.6	39.6	29.6	29.1	46.3	34.9	34.4	49.0
Asilimia ya Idadi ya Watu wa Vijijini	76.9	77.4	60.4	70.4	70.9	53.7	65.1	65.6	51.0

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu: Sensa ya watu na Makazi ya mwaka 2002, 2012 na 2022



## 5.0 Afya

### Idadi ya Vituo vya Kutolea Huduma ya Afya kwa Aina, Tanzania Bara, Mwaka 2018 - 2022

Aina ya Vituo	2018	2019	2020	2021	2022
Hospitali	285	294	369	404	418
Vituo vya Afya	834	910	926	956	1,016
Zahanati	7,000	7,242	7,163	7,189	7,447
<b>Jumla</b>	<b>8,119</b>	<b>8,446</b>	<b>8,458</b>	<b>8,549</b>	<b>8,881</b>

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

### Idadi ya Vitanda Katika Vituo vya Kutolea Huduma za Afya, Tanzania Bara, Mwaka 2021 and 2022

Aina	2021				2022			
	Serikali	Shirika la kujitolea/Dini	Binafsi	Jumla	Serikali	Shirika la kujitolea/Dini	Binafsi	Jumla
Hospitali ya Taifa	1,664	-	-	1,664	1,731	-	-	1,731
Hospitali Maalumu za Kibingwa	1,532	-	-	1,532	1,396	-	-	1,396
Hospitali za Rufaa za Kanda	2,407	-	-	2,407	1,059	860	-	1,919
Hospitali za Mikoa	7,239	898	420	8,557	6,688	-	-	6,688
Hospitali za Wilaya	10,636	6,228	409	17,273	3,033	7,425	-	10,458
Hospitali nyingine	1,098	10,395	2,915	14,408	14,510	1,086	21,412	37,008
Vituo vya Afya	14,363	4,939	2,105	21,407	17,151	1,695	5,968	24,814
Zahanati	14,462	1,863	2,558	18,883	14,811	158	5,704	20,673
<b>Jumla</b>	<b>53,401</b>	<b>24,323</b>	<b>8,407</b>	<b>86,131</b>	<b>60,379</b>	<b>11,224</b>	<b>33,084</b>	<b>104,687</b>

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

**Kiwango cha Uzazi na Kiwango cha Kuzaliwa kwa Makazi, Tanzania, 2022 TDHS-MIS**

<b>Makazi</b>	<b>Kiwango za Uzazi</b>	<b>Kiwango cha Kuzaliwa</b>
<b>Tanzania</b>	<b>4.8</b>	<b>33.8</b>
Tanzania Bara	4.8	33.8
Tanzania Zanzibar	4.7	32.9
<b>Tanzania Bara</b>		
Mijini	3.6	31.9
Vijijini	5.5	34.6

Chanzo: Ofisi ya taifa ya takwimu; Utafiti wa afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mmwaka 2022

**Mwenendo wa Kiwango cha Uzazi, Tanzania**

<b>Mwaka</b>	<b>Kiwango cha Watoto (watoto/mwanamke)</b>
Utafiti wa afya ya Uzazi na Mtoto 2004/05	5.7
